Msururu wa

# UPOTOFU NA UDANGANYIFU

Upotoshaji wa maana ya neno la Allah Alietukuka:

**( Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri )**

Kwa Vipote Vipotofu

Toleo

1

Sw

SANAD

بسم الله الرحمن الرحيم

Kila jinsi ya sifa njema ni za Allah Mlezi wa viumbe wote,
Rehma na Amani zimshukie mbora wa Manabii na Wajumbe,
Nabii wetu Bwana Muhammad na Jamaa zake na Swahaba zake wote.

# KISIMAMO CHA KUZINGATIA

Ni nini maana ya neno lake Allah alietukuka:

﴿Na ambae hatakuhumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾, ﴿Madhalimu﴾, ﴿Mafaasiq﴾[1]

Je wataraji maana ya Aya iwe ni kusisitiza kutekeleza hukmu ya Allah hata kama ni kwa vita? na je wafikiria Waislamu wapigane kwa ajili ya kutekeleza Aya hini? lakini kuna waliofahamu hivo! basi ni nani hawa walioifahamu hivi? na je wameifasiri vp? na je ndio ufahamu swahihi?

**S: Vp wamefahamu Vipote vipotofu Aya hini?**

Wahubiri wa Vipote vipotofu kwa jina la Uisilamu waona kua ambae hahukumu kwa Sharia ya Allah ni Kafiri yapasa kupigwa vita na ni halali kumuua, bali yule anaemchagua mtu kuhukumu nchi yake si kwa sharia ya Allah anazingatiwa ni Kafiri, na yule anaetegemea Qanuni za kuwekwa katika mambo yake ni Mshirikina! na maoni haya msingi wake ni ufahamu wao wa Aya: ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾.



**S: Nini natija ya Ufahamu huu mgonjwa?**

- **Kukufurisha aghlabiya ya Umma wa kiisilamu na kuwapa sifa ya Ushirikina wa Kijahiliya.**
- **Kulingania kuwakufurisha Wasmamizi wa Waisilamu.**
- **Kutokeza kwa Vipote vya Jihadi ya kukufurisha vilivoendelea kufikia kipote cha Daish wa sasa.**
- **Kujipatia vipengee vya vita na umwagaji wa damu kwa kisingizio cha kuhukumu kwa aliyoyateremsha Allah.**

(1) Sura ya Al-Maaida (44, 45, 47)

# WAKATI GANI ILIKUA MWANZO WA UFAHAMU HUNU MGONJWA?


Mwanzo : Kitone cha Mwanzo



## Abul Aalal Al-Maududy 1321 - 1399 H 1903 - 1979 M

Aliposema kwa Ufahamu wake kama alivopokewa kuhusu zile Aya tatu zilizofungamana na hukmu ya Allah Alietukuka : Hakika Qur'aani yasema kua kila hukmu kinyume na hukmu ya Allah sio kosa au haramu tu, bali ni Kufru na Upotevu na Udhalimu na Ufaasiq, na hukmu yoyote kama hiyo ni hukmu ya Kijahiliya, mtu hawi Mu'mini mda hajaikanusha. (2)

Pili : Kifungamanishi cha utenda kazi wa Viwanjani




## Sayid Qutbi 1324 - 1386 H 1906 - 1966 M

Ilikua juu ya kilele cha maoni ya Sayid Qutbi fikra ya Hakimiya, alio ichukua kutokana na fikra za Abil Aalal Al-Maududy, ila yeye aliipanua na akajengea juu lake mambo ya khatari, na akaweka nyongeza zake za kimaajabu alipozigusia Aya husika, na kuijalia pamoja na matawi yake ni mambo ya kiitikadi kwenye uisilamu, na akatoa hukmu kupitia hayo kwa asiehukumu kwa alioyateremsha Allah kua ni Kafiri, hata akiitakidi kua ni haki, na kua ni Wahyi [Ujumbe] kutoka kwa Allah. (3)

Na inadhwihiri wazi hayo katika maneno yake katika kutafsiri neno la Allah: ﴿Na abaye hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾﴿Maafasiq﴾ Wakati anaposema : Na hini sifa mpya haimaanishi kua ni hali nyengine kando na ile iliotangulia na sifa ya ukafiri katika neno lake Alietukuka:﴿Na ambaye hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾. ila inamaanisha kuongezea sifa nyengine kwa asiehukumu kwa alioyateremsha Allah, hua ni Kafiri kwa kumzingatia amekataa uola wa Allah Alietukuka na kupwekeka kwake katika kuwaekea Sharia waja wake na kwa kudai yeye haki ya uola kwa kudai haki ya kuwaekea watu Sharia. (4)

Tatu : Kusaidia na Kutilia nguvu



## Muhammad Qutbi 1337 - 1435 H 1919 - 2014 M

Kubuni Sharia sio kwa aliyoyateremsha Allah na kuridhia Sharia inayopingana na aliyoyateremsha Allah yote mawili - katika hukmu ya Allah - ni kutangua [neno] Hapana Mola anaestahiki kuabudiwa Ila ni Allah ndio mana ikateremka juu ya hilo hukmu ya kukata na kuamua: ﴿Na ambaye hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾ (5)

Basi angalia vp ulikuja ufahamu hunu usiohusiana na ufahamu wa waliotangulia juu ya Aya zile kwa namna hii ya kimaajabu, tena katika zama za kuchelewa, iliopelekea kuwahukumia Umma mzima Ujahiliya na Ukafiri!



(2) Al-Khilafa Wal Mulk cha Abul Aalal Al-Maududy

(3) Angalia Dhwilal Al-Qur'an cha Sayid Qutbi 2 | 887 17

(4) Dhwilal Al-Qur'an 2/900

(5) Mafahim yajib An Tuswahah | 118

## KISIMAMO
## CHA KUHAKIKISHA

**Je Ufahamu uliotangulia walingana na Muongozo wa Mtumi na Ufahamu wa Maswahaba na Waliotangulia wema na Wanvyuoni wa Umma?**

Zama za Mtumi

Wapi na ni kwa nani iliteremka Aya hini Tukufu?



Iliteremka Aya Tukufu iliotangulia Madina Inayo'ngaria wakati Mayahudi walipomuuliza Mtumi Rehma na Amani ziwe juu yake kuhusu waliozini wakiwa wameowa, na zote ziliteremka juu ya Makafiri. (6)

Tafsiri ya Mfasiri. Mwanachuoni. : Bw. Abdallah Ibnu Abbaas R. A. 17 H

---

Amepokea Twauss kutoka kwa Ibni Abbaas katika neno lake [Mungu] : ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾ , Alisema : "Sio Ukafiri ule wanao ukusudia" na katika tamko lengine : "Ukafiri usiotoa ndani ya Milla [ya Kiisilamu]" na katika tamshi : "Ukafiri chini ya Ukafiri na Udhalimu chini ya Udhalimu na Ufaasiq chini ya Ufaasiq". (7)

## KUKOSOA NA KUREKIBISHA

Je kuna Ugomvi juu ya Tafsiri na Ufahamu wa Ibnu Abbass Juu ya Aya hini, na una uzito gani Ugomvi huo?



- Ukosowaji wa Kwanza : Mategemezi ya Upokezi uliotangulia kuna Hisham bin Hujeyr, na kuna waliomdhofisha?
- Jawabu : Yatosha kumtilia nguvu Hisham bin Hujeyr kua Bukhari na Muslim wanamtegemea katika Swahihi zao. kisha Imam Sufyan Al-Thawry alimfuatilia Hisham bin Hujeyr , na amepokea kwake Mapokezi haya Imam Sufyan bin Uyayna. (8)
- Ukosowaji wa pili : Ibara " Ukafiri chini ya Ukafiri" ni katika maneno ya Twaaus wala sio maneno ya Ibni Abbaas kwa Upokezi wa Abdur-Razzaq?
- Jawabu : Aliepokea Ibara hini kutoka kwa Ibni Abbaas ni Sufyaan bin Uyeyna, na yeye ni mjuzi zaidi kuliko Abdur-Razzaq hivo anamtangulia. na huo ni Upokezi wa Hakim katika Mustadrak aliousahihisha na akamuafiki yeye Al-Dhahaby katika hilo. (9)

**Natija :** Ukosowaji hunu hauna nguvu wala hausimamishi hoja ya kuirudi Tafsiri ya Ibni Abbaas juu ya Aya hini tukufu.

(6) Asbabun Nuzul 1|195 cha Abil Hasan Ali Al-Wahidy An Naysabury , Zadul Muyasar 1|551 cha Abil Faraj Abdurahman Aljawzy , Muslim 3|1700

(7) Ameitolesha Muhammad bin Nasr Al-Mirwazy 294 H katika Mlango (Taadhim Qadris Swalaa) 2|521|574|575 .

(8) Tahdhibut Tahdhib - (34 / 33)

(9) Ameitolesha Hakim katika Mustadrak (Tafsiru Suratul Maaida) 2/342/ Hadith : 3219

## WALIIFAHAMU VP WANAVYUONI WAKUBWA AYA HINI?

### Imaam Ahmad bin Hanbal 241 H

Amesema Ismail bin Saad: nilimuuliza Ahmad kuhusu neno lake [Allah] Alietukuka: ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾ nikasema ni Ukafiri upi huu? akasema: "Ukafiri usiotoa ndani ya Milla [ya Kiisilamu]". (10)

### Imaam Ibnu Abdil Bar 463 H

"Na wameafikiana Wanavyuoni kua kuhukumu vibaya ni katika dhambi kubwa kwa anaekusudia huku akijua, imepokewa juu ya hilo nukuu kali kutoka kwa waliotangulia. na amesema Allah Alietukuka: ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾ , ﴿Madhalimu﴾, ﴿ MafaasiQ﴾ .
ziliteremka kwa Ahlul-Kitaab, na Amesema Hudheifa na Ibnu Abbaas: "Ni kwetu sote" wakasema: "Sio Ukafiri unaotoa ndani ya Milla [ya Kiisilamu] anapofanya hilo mtu katika Umma hunu, paka iwe atakanusha Allah na Malaika wake na vitabu vyake na Wajumbe wake na Siku ya mwisho" (11)

### Imaam Qurtubiy 671 H

" Na neno lake [Allah] Alietukuka: ﴿Na ambae hatahukumu kwa aliyoyateremsha Allah, basi hao ndio Makafiri﴾ wanasimamisha hoja kwa maana yake ya nje wanaokufurisha [watu] kwa madhambi nao ni Makhawarij, wala hawana hoja ndani yake, sababu Aya hini iliteremka juu ya Mayahudi wanaobadilisha maneno ya Allah Alietukuka, kama ilivokuja kuzungumzia hilo hadithi, nao ni Makafiri, hivo watashirikiana nao katika hukmu yake wanaoshirikiana nao katika sababu ya kuteremka kwake". (12)

## JE WAMEAFIKI WANAVYUONI WENGI TAFSIRI YA IBNU ABBAAS R. A. KATIKA AYA HINI?

Imeafiki ufahamu wa Wanavyuoni wengi wa umma Aya hini kua ni: (Ukafiri chini ya Ukafiri) yani hawi kafiri kwa hilo mwenye kufanya hivo, Ufahamu wa Mwanachuoni Bingwa wa Umma Bwana wetu Abdallah bin Abbaas kutokana na Mabwana Maimamu na Wanavyuoni bora, Kati yao kwa njia ya mfano sio wote :

| | |
|---|---|
| Abdur-Razzaq bin Humam As Swanaaniy | 211 H - Tafsiir As-Swanaaniy |
| Abi Muhammad A. bin Abi Hatim Ar-Raziy | 277 H - Tafsiir Ibnu Hatim |
| Ibnu Jurayr At-Twabariy | 310 H - Jamiul-Bayan |
| Ahmad bin Ali Abubakar Ar-Raziy Al-Jaswas | 370 H - Ahkamul-Qur'an |
| Muhammad bin Ahmad Al-Qurtubiy | 468 H - Al-Jaamiu |
| Imaam Abu Mudhwafar As-Samaaniy | 489 H - Tafsiir As-Samaaniy |



(10) Sualat Ibnu Hani'i 2|192 .
(11) At-Tamhiyd 5|74 .
(12) Al-Mufham Lima Ashkala Min Talkhis Muslim cha Abi Al-Abbaas Ahmad Al-Qurtubiy 2|116 .

| | |
|---|---|
| Muhamad bin Nasr Al-Mirwaziy | 294 H - Taadhwim Qadris-Swala |
| Abdul-Haq bin Atwiya Al-Andalusiy | 541 H - Al-Muharar Al-Wajiz |
| Abubakar Muhammad bin Abdallah Al-Maafriy | 543 H - Ahkamul-Qur'an |
| Abul-Faraj bin Al-Jawziy | 597 H - Zadul-Masiyr |
| Muhammad Umar At-Tiymiy Al-Bikriy Ar-Raziy | 606 H - Tfsir Ar-Raziy |
| Abul-Abbaas Ahmad bin Umar Al-Qurtubiy | 656 H - Al-Mufhim |
| Al-Husein bin Masuud Al-Baghawiy | 516 H - Maalimut-Tanziyl |
| Abdallah bin Ahmad An-Nasafiy | 710 H - Tafsiir An-Nasafiy |
| Ahmad Ibnu Taymiya | 738 H - Fatawa Ibnu Taymiya |
| Ali M. Ibrahim As-Shayhiy Alaaud-Din | 741 H - Tafsir Al-Khaazin |
| Muhammad Y. bin Hayaan Al-Andalusiy Al-Nafriy | 745 H - Tafsiir Al-Bahrul-Muhiyt |
| Muhammad M. Jaziy Al-Kalbiy Al-Gharnatwiy | 741 H - At-Tashiyl Fi Ulumit-Tanziyl |
| Abu Ishaaq Ibrahim bin Musa Ashaatwibiy | 790 H - Al-Muwafaqat |
| Ibnu Abil-Izz Ali bin Alaad-Din Al-Dimashqiy | 793 H - Sharhul-Aqiydat-Twahawiya |
| Al-Qadhwiy Abus-Suud | 983 H - Tafsiir Abus-Suud |
| Muhamad Swadiq Khaan | 1307 H - Fathul-Bayaan |
| Muhammad Ali As-Shawkaniy | 1355 H - Fathul-Qadiir |
| Ahmad Mustwafa Al-Maraghiy | 1371 H - Tafsir Al-Maraghiy |
| Shaikh Abdur-Rahman bin Naasir As-Saadiy | 1376 H - Tafsiir As-Saadiy |
| Muhammad Al-Amiin As-Shanqiytwiy | 1393 H - Tafsiir Adhwaaul-Bayaan |

Na Baada maonesho haya ya maneno ya Wanavyuoni wa Ahlu Sunna wal Jamaa, pia Ufahamu wa Wanavyuoni wanaowaregelewa kwa sasa na wenye fikra inayomkufurisha asiehukumu kwa aliyoyateremsha Allah unapingana nao, kama vile Al-Baaniy katika (Silsilatu Swahihul-Al-Baaniy juzu ya 6 kurasa ya 106)
Na Ibnu Uthaimiin katika (Alt-Tahdhiir Min Fitnatit-Takfiir kurasa ya 68) .

## NATIJA YA FAHAMU POTOFU

- Imewapelekea kupita mipaka ya Kisharia vibaya kwa kuwakufurisha wasmamizi wa Waisilamu.
- Kuwakufurisha walioridhia hukmu za wasmamizi hao na kutaka hukmu kwao au alowanyamazia kati ya Waisilamu.
- Kupingana na Ufahamu wa na Maoni ya Waliotangulia wema kutokana na Maswahaba na waliowafuatia na Wanavyuoni wa Umma kama ulivyoona.
- Kuenea Mauwaji na Kuhalalisha umwagaji damu na kutowa rohozilizohifadhiwa na kujipatia vipengee vya vita vya ndani kwa kisingizio cha kuhuisha Khilafa na kuhukumu kwa aliyoyateremsha Allah.

## NATIJA YA FAHAMU ZA WANAVYUONI WA UMMA

- Fahamu potofu juu ya Aya hini inaafikiana na Fahamu ya Khawarij wa karne ya kwanza.
- Anaehukumu kwa sio aliyoyateremsha Allah kwa kusudi anafanya Maaswiya na Makosa Allah atamlipa na ni katika dhambi kubwa.
- Anaefanya hivo hatoki katika mzunguko wa [Dini ya] Uiisilamu.
- Anaefanya hivo bado ni Muisilamu aliyehifadhiwa damu yake.
- Inapasa Wanavyuoni wamnasihi na wamlekeze kwa vizuri

"Na ujue kua Khawarij wanatolea dalili Aya hini kua asiehukumu kwa aliyoyateremsha Allah ni Kafiri, na Ahlu Sunna wamesema hawi Kafiri kwa kuacha kuhukumu [kwa aliyoyateremsha Allah]" (13)

Imaam As-Samaaniy

(13) Tafsiri ya Imaam As-Samaaniy 2|42 .

# MSURURU WA
# UPOTOFU NA UDANGANYIFU

Amesema Mjumbe wa Allah Rehma na Amani ziwe juu yake na jamaa zake: (wataichukua hini Elimu [Dini] Waadilifu katika kila watakaokuja, watakao itetea kutokana na Upotofu wa Wenye kuzidisha na Udanganyifu wa Wenye kuharibu na Ufafanuzi wa Wajinga).
[Hadithi mash'huri ameiswahihisha Ibn Abdil Bar, na amepokewa Ahmad bin Hanbal kua Amesema: hio ni Hadithi Swahihi]

Wamefahamu baadhi ya wenye fikra za makosa, maneno ya Allah Mtakatifu kwa namna hailingani na mfumo wa kielimu uliopokewa kutoka kwa waliotangulia wema, wala kuchukuana na makusudio na misingi mikubwa ya Ujumbe wa Mungu.

Wakazichukua kusudi baadhi ya Aya za Qur'aani Tukufu ambazo ziliteremka kwa wasiokua Waislamu, wakaziteremsha kwa Waislamu. Na wakachukua Aya ambazo zimekuja si kwa jumla wakazifanya ni Maagizo ya kwa jumla.
Na wakapotosha maana ya maneno ya Allah kwa namna imepelekea kukita kwa ufahamu wa kimakosa sana ndani ya akili za Waislamu wasiowasomi, uliowapelekea kwenye nyendo na vitendo havina ufungamano na Dini ya Unyenyekevu ya Kiislamu.

Tutajua kupitia vifungu vya msururu huu ulioshikana, upotoshaji wa maana ya Aya za Qur'aani Tukufu, waliouangukia wenye fikra hizi potofu na vile uilivoepukana [Ufahamu wao] na ufahamu wa Mtumi Mtukufu Rehma na Amani ziwe juu yake na Jamaa zake na Swahaba zake na Waliotangulia wema na Sharia [ya Kiislamu] inayo n'garia.

SANAD
www.sanad.network
twitter: @sanadnetwork
facebook.com/sanadnetwork
youtube.com/sanadnetwork
دار الفقيه للنشر والتوزيع
DAR AL FAQIH
PUBLICATION & DISTRIBUTION